


# Masasisho ya taratibu za kujiandikisha

Taarifa kwa familia

## Je, ni kitu gani kimebadilika?

Mabadiliko yafuatayo yamefanywa kwa taratibu za Kuandikisha katika Chekechea (Kindergarten) hadi Mwaka wa 12 (Year 12) na hutumika kwa uandikishaji wote wa shule za umma unaoanza katika Kipindi cha 1, 2026.

### Masasisho ya kujiandikisha kusiko kwa wenyeji (mahali husika)

Katika 2025, tulianzisha vigezo vya kuweka kipaumbele maombi ya uandikishaji usio wa wenyeji kwa wanafunzi wenye mahitaji fulani ya kujifunza na ustawi, wadogo na wakubwa wa wanafunzi ambao wameandikishwa kwa sasa, na watoto wa wafanyakazi wa shule.

Katika 2026, kujiandikisha kwa nje ya eneo kutapewa kipaumbele pia kwa ajili ya:

- Wanafunzi wa Asili na/au Wanavisiwa wa Torres Strait ili kutambua mahusiano ya kitamaduni, kifamilia na kinship connections.
- Wanafunzi wanaoingia Kindergarten ambao wamehudhuria shule ya awali ya umma iliyopo pamoja na shule ya umma ya NSW.

### Unyumbufu zaidi kwa watoto wa Wanajumbe wa Jeshi la Ulinzi

Taratibu za kuandikisha zinasasishwa ili kuhakikisha urahisi zaidi wa kubadilika mahitaji ya uandikishaji shuleni kwa watoto wa Wanajumbe wa Jeshi la Ulinzi wakati wa kuhama na wakati wa kupata makazi.

### Kutambua kinship za Asili na/au za Wanavisiwa wa Torres Strait

Shule zitakuwa na uwezo wa kubadilika zaidi kuandikisha wanafunzi wa Asili na/au Wanavisiwa wa Torres Strait, ikiwa ni pamoja kwa kinship connections, usalama wa kitamaduni, upatikanaji wa masomo ya lugha ya Asili na majukumu ya kitamaduni kama vile Sorry Business.

### Muendelezo kwa wanafunzi wetu walio katika mazingira magumu zaidi

Mwongozo maalum kwa wanafunzi walio kwenye dhamana na wanafunzi wanaohama kutoka shule katika vituo vya haki za vijana na mahabusu unajumuishwa pia na maombi ya kuandikisha kwa eneo kwa wanafunzi wa kigezo hiki yatashughulikiwa ndani ya siku 2 za shule.

## Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

### Je, mabadiliko hayo yanamhusu mtoto wangu?

Mabadiliko ya 2026 ya taratibu za kuandikisha katika shule za umma za NSW yanakuhusu ikiwa:

- mtoto wako ni wa Asili na/au ni Mwanavisiwa wa Torres Strait mwenye mambo ya kuzingatia kinship, kuhusu lugha au utamaduni
- mtoto wako amekuwa katika uangalizi wa nje ya nyumba, kwa dhamana, au anahama kutoka shule katika vituo vya haki za vijana na mahabusu
- mmojawapo wa wazazi wa mtoto wako amehudumu au kwa sasa anahudumu katika Jeshi la Ulinzi na anaweza kuathirika na mahitaji ya kuhama kutokana na kufanya kazi kwa Jeshi la Ulinzi wa Australia.

### Je, kila shule atahitajikwa kutumia mabadiliko hayo?

Kulingana na upatikanaji wa uandikishaji wa shule, shule zinahitajika kutumia mabadiliko kwa uandikishaji usio wa wenyeji kwa wanafunzi wanaojiandikisha kwa Kipindi cha 1, 2026.

Mabadiliko ya taratibu za kuandikisha kwa wanafunzi wasio wenyeji hayataathiri mahitaji ya kustahiki ya mipangilio au programu maalum, kama vile shule zinazochaguliwa kabisa, shule kwa madhumuni maalum (schools for specific purposes (SSPs)), shule za elimu ya mbali, na shule zenye madarasa au miradi yenye mahitaji maalum ya ustahiki (kwa mfano madarasa ya fursa, mikondo ya michezo maalum na/au sanaa ya ubunifu au maonyesho). Shule hizi zinakabiliwa na taratibu zao, vigezo vya ustahiki na tathmini na zitaendelea kufuata michakato yao ya uandikishaji ya sasa.

Shule za jinsia moja lazima zitumie mabadiliko mradi tu mtoto anayejiandikisha anakidhi mahitaji ya shule ya kustahiki kwa jinsia hiyo. Wasiliana na shule husika kuuliza jinsi mabadiliko haya yanavyotumika.

### Je, ombi langu la uandikishaji usio wa wenyeji litakubaliwa moja kwa moja ikiwa mtoto wangu anakidhi vigezo vilivyosasishwa?

Mabadiliko hayo hayahakikishii mtoto wako kuandikishwa katika shule ya umma isiyo ya eneo lako. Shule ambazo zina uandikishaji wa nje na ndani ya eneo zitazingatia ombi lako. Shule ambazo zina upatikanaji mdogo wa uandikishaji usio wa wenyeji zitaweka kipaumbele uandikishaji usio wa wenyeji kwa:

- wanafunzi wenye mahitaji ya kujifunza na ustawi wanaohitaji marekebisho yanayofaa na/au usaidizi wa ziada wa kielimu, ikiwa ni pamoja na
  - wanafunzi wa Asili na/au wanavisiwa wa Torres Strait wenye mambo ya kitamaduni na/au familia na kinship connections na mahusiano
  - Ulemavu
  - Umri wa ukuaji
  - Kiwewe
  - Masuala ya ulinzi wa mtoto
  - Mahitaji na hali ya kimatibabu na kibinafsi
- wadogo na wakubwa wa tumbo moja wa wanafunzi wanaohudhuria shuleni kwa sasa, na wadogo na wakubwa wa wanafunzi katika vitengo vya usaidizi hupewa kipaumbele
- mwanafunzi anayeingia Kindergarten ambaye amehudhuria shule ya awali ya umma iliyopo pamoja na shule ile.

Wasiliana na shule husika kupata taarifa zaidi.

### Je, ina maana yake wanafunzi ambao wanaridhi tu vigezo vya kipaumbele kwa uandikishaji usio wa wenyeji watakubaliwa kuanzia sasa?

Hapana, wazazi wanakaribishwa kutuma maombi ya kuandikisha mtoto wao kwa shule yoyote ya umma ikiwa mtoto anastahiki kuhudhuria shule ile na shule inaweza kujumuisha mtoto katika upatikanaji wake wa kuandikisha Shule zote ambazo zina upatikanaji mdogo usio wa wenyeji lazima ziweke kipaumbele na huzingatia maombi kulingana na vigezo vilivyosasishwa vya uandikishaji usio wa wenyeji.

### Ombi langu la awali la uandikishaji usio wa wenyeji lilikataliwa, lakini mtoto wangu anakidhi vigezo vilivyosasishwa sasa. Je, naweza kutuma ombi tena?

Ndiyo. Ikiwa ulituma ombi kwa mtoto wako kwenda kwa shule isiyo ya wenyeji katika 2026 na ombi lilikataliwa, unaweza kuomba tena ikiwa mtoto wako anakidhi vigezo vilivyosasishwa vya uandikishaji usio wa wenyeji. Tafadhali fuata hatua zilizoelezwa katika sehemu hapa chini, "Je, nibadilishaje mahali nilipomwandikisha mtoto wangu?".

### Nimewasilisha Onyesho la Nia (Expression of Interest (EOI)) kwa Mapito ya Year 6 hadi 7. Je, naweza kubadilisha mahali ambapo nimeandikisha mtoto wangu?

Ndiyo. Ikiwa mtoto wako anakidhi vigezo vilivyosasishwa vya uandikishaji usio wa wenyeji, unaweza kutuma maombi mapya kwa shule unayopendelea isiyo ya eneo lako, hata kama tayari umewasilisha EOI ya mapito ya Year 6 hadi 7. Tafadhali fuata hatua zilizoelezwa katika sehemu hapa chini, "Je, nibadilishaje mahali nilipomwandikisha mtoto wangu?".

### Je, nibadilishaje mahali nilipomwandikisha mtoto wangu?

Wazazi au walezi ambao wangependa kumwandikisha mtoto wao katika shule isiyo ya wenyeji wanahitaji kufuata hatua hizi kubadilisha uandikishaji wake:

**Maombi ya kuandikisha mtandaoni**

1. Nenda kwenye tovuti ya shule ya umma unayotaka kutuma ombi la kuandikisha, kisha bonyeza kwa kuandikisha (enrolment) katika chaguzi za menyu.
2. Kwenye ukurasa wa tovuti wa kuandikisha, chini ya kichwa cha jinsi ya kuandikisha (how to enrol) bonyeza kwenye kiungo kwa ombi la kuandikisha mtandaoni (online enrolment application).
3. Mara baada ya kuwa umewasilisha ombi lako la kuandikisha, shule inaweza kukupa ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa, wasiliana na shule ambayo mtoto wako aliandikishwa hapo awali ili kuondoa uandikishaji huo.

**Maombi ya fomu ya karatasi**

1. Wasiliana na shule isiyo ya wenyeji ili kujua kama inaweza kumjumuisha mtoto wako.
2. Ikiwa shule inaweza kumjumuisha mtoto wako, tafadhali jaza fomu mpya ya ombi la karatasi ambayo shule inaweza kuitoa.
3. Mara baada ya kuwa umewasilisha ombi lako la kuandikisha, shule inaweza kukupa ofa ambayo utahitaji kukubali ndani ya siku 14.
4. Ikiwa ombi lako linakubaliwa, wasiliana na shule ambayo mtoto wako aliandikishwa hapo awali ili kuondoa uandikishaji huo.

## Je, itakuwaje kama sina anwani ya kudumu au nyaraka zinazohitajika za utambulisho?

Kuna hali ambazo mwanafunzi anaweza kujiandikishwa bila uthibiti ya anwani. Hali hizi zinajumuisha, lakini haziishii tu kwenye, mambo ya kitamaduni, watoto wa Wanajumbe wa Jeshi la Ulinzi na watoto au vijana katika uangalizi wa nje ya nyumba, kwa dhamana, au wanahama kutoka shule katika vituo vya haki za vijana na mahabusu. Tafadhali wasiliana na shule husika kupata maelezo zaidi ikiwa unaona kuwa hii inaweza kutumika kwa hali yako.

## Je, mabadiliko ya sera na taratibu za kuandikisha ya 2025 bado yanatumika?

Ndiyo. Mabadiliko yaliyoanzishwa katika 2025 yataendelea kutumika kwa uandikishaji wa 2026. Hayo yanajumuisha:

- Wanafunzi wote wenye viza ya mkazi ya muda wanaweza kujiandikisha katika shule ya umma ya eneo lao, kulingana na anwani yao ya makazi.
- Wadogo na wakubwa wa tumbo moja wa wanafunzi ambao wameandikishwa kwa sasa katika shule ya umma wanapewa kipaumbele kwa uandikishaji usio wenyeji, na kipaumbele kinatolewa kwa wadogo na wakubwa wa wanafunzi wa madarasa ya usaidizi katika shule zinazostahiki za kawaida.
- Watoto wa wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatiwa kwa uandikishaji usio wa wenyeji katika shule ya umma.

Kupata taarifa kuhusu mabadiliko hayo, au kuangalia ikiwa yanatumika kwa mtoto wangu, wasiliana na shule husika.

## Je, niwezaje kupata maelezo zaidi?

**Kwa maswali ya kuandikisha, zungumza na shule unayopendelea. Pata maelezo ya mawasiliano ya shule yako kwa:**
education.nsw.gov.au/find-a-public-school

**Kwa taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kujiandikisha katika shule ya serikali ya NSW:**
education.nsw.gov.au/enrolment

**Kwa taarifa zaidi kuhusu jinsi ya kujiandikisha katika shule ya serikali ya NSW kama Mkazi wa Muda:**
https://www.deinternational.nsw.edu.au/

**Kwa maswali ya kuandikisha kwa jumla, wasiliana na ofisi kuu ya Idara ya Elimu:** 1300 679 332

**Huduma ya Mkalimani wa Simu**

Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kuwasiliana na shule au Idara ya Elimu, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 13 14 50 na uliza kupata mkalimani katika lugha yako. Mwambia mpigaji simu nambari ya simu unayotaka kupiga simu na mpigaji simu atapata mkalimani kwenye simu kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.